Mungu Aliumba Ulimwengu
(God Made the World)

Kimetafsiriwa kwa Kiswahili na Xavery Ngullo

(Translated into Swahili by …)

Kitabu kimehaririwa na: T.L.G. Raynor

(Edited by …)

Page 1 (note to parents)

Kwa Wazazi

Waandikaji wa Utetezi (Apologetics Press), ni shirika lisilo la biashara limejitolea kwa ajili ya utetezi wa Ukristo wa Agano Jipya. Kwa zaidi ya robo-karne tumetengeneza vitu vingi vya kujenga imani ya watu wazima. Na tumezalisha vitu vingi kama vile Ugunduzi (Discovery), Safu za Mtafiti (Explorer), na baadhi ya vitabu kwa ajili ya vijana wa daraja la tatu shule za sekondari. Na sasa tumependezwa kutoa safu mpya ya vitabu hata kwa watoto wadogo zaidi.

Shirika la "Apologetics Press Early Reader Series" (Waandishi wa utetezi kwa Safu ya mwanzo ya Msomaji) ni vitabu vilivyolengwa kwa watoto katika shule za chekechea, mpaka darasa la pili. Inategemea umri wa watoto wako, safu hii inaweza kumwezesha mzazi kuchagua kuwasomea watoto wao, au kusoma pamoja na watoto wao au kusikiliza wanaposoma watoto wao, wanaposoma kwa sauti kubwa.

Vitabu vya safu hii vimejaa picha za rangi mzuri na dhahiri na habari nzuri kuhusu Mungu, Viumbe Vyake, na neno Lake. Vitabu hivi vimeandikwa kwa kiwango ambacho wasomaji wapya watakifurahia, na hilo litawavutia kwa Muumbaji wao.

Tunategemea kuwa mtaifurahia kutumia safu hii ya Waandishi wa safu za Mwanzo za Msomaji kuwafundishia watoto wenu, kusoma, kwa wakati huo huo wakijifunza kuhusu Mungu na viumbe Vyake.

Page 2

Mungu Aliumba Ulimwengu
Na Kyle Butt
Kimeandikwa (Copyright ©) 2005
Apologetics Press
Haki zote zimehifadhiwa.
Hakuna ruhusa ya kunukuu sehemu ya kitabu hiki kwa namaa yoyote bila kibali cha mhariri wa kitabu.
ISBN: 0-932859-69-0
Maktaba ya Congress: 2005926995
Kimepigwa chapa nchini China.

Page 3

Mungu Aliumba Ulimwengu
Na Kyle Butt

Page 4

Siku ya Kwanza
Katika siku ya kwanza Mungu aliumba dunia.
Ilikuwa imefunikwa kwa maji.
Dunia ilikuwa na giza sana.

Page 5

Alitenganisha
nuru na giza.
Akaiita giza Usiku.
USIKU

MCHANA
Mungu pia aliumba Nuru.
Akaiita nuru Mchana.

Page 6

Siku ya Pili
Katika siku ya pili Mungu aliumba anga na hewa.
Wanyama na watu wanavuta hewa.
Bila kuwepo anga na hewa, wanyama na wanadamu wasingeweza kuishi.

Page 7

Siku ya Tatu
Mungu aliumba nchi kavu katika siku ya tatu.
Katika nchi kavu Mungu aliweka miti, maua na mimea.
Alifanya aina tofauti za mimea.

Page 8

Baadhi ya mimea ni midogo na hutoa maua mazuri sana.
Tazama ua hili lilivyo zuri.

Page 9

Mimea mingine ni mikubwa, nayo hutoa matunda ambayo ni mazuri kwa kula.
Tazama matunda yote hayo matamu.
Je, waweza kutaja majina ya matunda hayo?

Page 10

Wanyama na wanadamu pia hupenda kula matunda.
Lakini katika siku ya tatu ya uumbaji hapakuwepo wanadamu wala wanyama.
Mungu alikuwa hajawaumba bado.
Je, unaweza kutaja majina ya matunda hayo?

Tunda-Nyota	Embe	Papai
Star Fruit	*Mango*	*Papaya*

Page 11

Siku ya Nne
Katika siku ya nne, Mungu aliumba Jua, Mwezi na nyota.

Page 12

Aliliweka Jua angani ili litawale mchana.
Aliuweka Mwezi angani ili utawale usiku.
Mungu aliziweka nyota angani ili ziangaze usiku.

Page 13

Jua
husaidia
mimea
kujitengenezea
chakula.

Mwezi
hudhibiti
kupwa
na
kujaa
kwa
maji
ya
bahari.

Page 14

Nyota zinaweza kutumika kuongoza meli.
Jua, Mwezi na nyota zinatusaidia kuhesabu muda.

Page 15

Dunia hulizunguka Jua kwa mwaka mmoja.
Mwezi mpevu huangaza mara moja tu kwa muda wa mwezi mmoja.

Page 16

Siku ya Tano
Mungu aliumba wanyama katika bahari katika siku ya tano.
Samaki waliumbwa Siku ya Tano

Page 17

Samaki wengine ni wadogo na wazuri kama hawa Samaki Wachekeshaji.
Page 18

Samaki wengine ni wakubwa na wabaya kama huyu anaitwa Chewa.

Page 19

Viumbe wengine wa baharini siyo samaki.
Pweza aliumbwa siku ya tano. Je, ana miguu mingapi?

Page 20

Papa pia waliumbwa siku ya tano.
Baadhi ya papa wana kasi wanapoogelea, wanayo meno mengi na wanakula samaki wengine.

Page 21

Nyangumi siyo samaki, lakini wanaishi bararini.
Nyangumi wengine ndiyo wanyama wakubwa kuliko wote ambao wanaishi sasa.

Nyangumi hawa ni wakubwa kama gari la kubebea mizigo.

Page 22

Mungu pia aliumba ndege na wanyama warukao siku ya tano.
Ndege wapo katika ukubwa mbalimbali na maumbile mengi.

Page 23

Ndege wengine ni wadogo na wazuri kama huyu ndegeuvumi.
Ndege wengine ni wakuwa na wala siyo wazuri sana kama huyu, Mumbi.

Page 24

Ndege kama Pengwini huogelea katika maji ya baridi.
Pengwini hawawezi kuruka juu lakini wanaweza kuogelea haraka.
Wanaishi palipo na barafu na theluji.

Page 25

Wanyama kama popo wanaweza kuruka.
Lakini popo siyo ndege.
Wanajitundika na kuning'inia kwenye mapango ya giza. Popo wengine huruka usiku na kula wadudu.

Page 26

Siku ya Sita
Mungu aliumba wanyama wa nchi kavu siku ya sita.

Page 27

Mtazame tembo mkubwa. Ana mkonga mrefu ambao huutumia kupata chakula. Pia anazo pembe ndefu.
Baadhi ya wanyama wa nchi kavu ni wakubwa sana.

Page 28

Wanyama wengine ni wadogo sana.
Angalia panya hawa wadogo kabisa.

Page 29

Baadhi ya wanyama huishi msituni.
Mtazame nyani akiwa mtini.
Mara nyingine nyani hutumia mikia yao kujishikilia matawini.

Page 30

Wanyama wengine huishi mashimoni ardhini.
Nguchiro huchimba nahandaki chini ya ardhi.

Page 31

Mungu pia aliumba wanadamu siku ya sita.
Adamu na hawa ndio waliokuwa wanadamu wa kwanza. Mungu alimuumba Adamu kwanza.

Page 32

Siku ya Saba
Mungu aliacha kuumba katika siku ya saba.
Mungu alipomaliza alisema kuwa kila kitu kilikuwa chema.

(Back Cover:)

Tunaanzisha A.P. Reader Series *(Introducing…)*

Moja kati ya mambo muhimu zaidi ambayo watoto wanaweza kujifunza ni kwamba Mungu aliumba ulimwengu. Biblia inasema, maana kwa siku sita Mungu alifanya mbingu na nchi na bahari na vyote vilivyomo, akastarehe siku ya saba, kwahiyo Bwana akaibarikia siku ya sabato akaitakasa (Kutoka 20:11). Alifanya jua liangaze na nyota kumeremeta angani. Aliumba samaki wanaogelea baharini, na ndege warukao angani. Alimuumba mwanadamu mwishoni japokuwa siye mdogo kuliko wengine, aliumba mtu wa kwanza pamoja na mwanamke pia—Adamu na Hawa.

Kuhusu A.P. Safu ya Wasomaji *(About the A.P. Reader Series)*

Kuna njia gani nyingine iliyobora ya kujifunzia kusoma kuliko kuanza kwa kusoma kuhusu Mungu na Uumbaji wake? Siyo tu kwamba watoto wenu watasoma kuhusu anga, miti, pamoja na wadudu, bali pia watajifunza kuhusiana na Mbunifu aliyefanya mambo hayo yote kwa maandishi ya kueleweka, picha, watoto wenu watapenda kusoma na pia Watampenda Muumbaji wao.